

Kamati ya Elimu, Afya na Huduma za Uchumi

Kamati ya Elimu, Afya na Huduma za Uchumi ni kati ya kamati tatu (3) za kudumu. Kamati hii hushughulikia mambo yote yanayohusu afya ya jamii, elimu na huduma za maji.

Kamati hii pia hushughulikia mambo yanayohusiana na jitihada za wananchi mitaani kujiletea maendeleo yao kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja kushauri, kushawishi, kuzindua, kuelimisha na kushirikisha wananchi hao hasa katika kutayarisha, kutekeleza, kusimamia na kutathmini mipango yao ya maendeleo.

Majukumu Maalumu ya kamati

- i. Kuandaa mipango madhubuti ya maendeleo ya upanuzi na ujenzi wa hospitali, vituo vya Afya na zahanati.
- ii. Kuandaa mipango ya maendeleo ya upanuzi na ujenzi wa shule za awali na msingi
- iii. Kupendekeza mipango ya upanuzi wa vituo vya Afya, viwanja, majengo na mazingira y burudani, starehe, mapumziko na michezo.
- iv. Kuamua juu ya mambo yanayohusu uhifadhi wa mambo ya kale na mandhari Mbalimbali yenyе sura nzuri.
- V. Kupendekeza kwa Halmashauri mipango ya kupanua biashara na jinsi ya kukusanya mapato yatokanayo na upanuzi huo.
- Vi. Kusimamia matumizi ya sheria ya nguvu kazi
- Vii. Kuandaa mipango madhubuti ya maendeleo ya upanuzi wa kilimo katika Halmashauri.
- Viii. Kushughulikia uanzishaji na uendelezaji wa vyama vya ushirika kwa Mujibu wa sheria ya vyama vya Ushirika.
- ix. Kuweka mikakati ya makusudi juu ya njia bora za kuchangia baadhi Ya huduma za Elimu na Afya.
- X. Kubuni na kupendekeza njia bora za kuzuia na kudhibiti magonjwa ya Mlipuko.
- Xi. Kuandaa na kuratibu njia bora juu ya uhifadhi wa nyaraka muhimu kwa Ajili ya kumbukumbu hizo zitahifadhiwa kwa mujibu wa sheria ya serikali za Mitaa Sura ya 288.
- Xii. Kupendekeza matumizi bora ya lugha ya taifa.
- Xiii. Kupendekeza njia bora juu ya uhifadhi wa sanaa mbalimbali za ufundi za maonesho kwa mujibu wa sheria ya serikali za mitaa sura ya 288
- Xiv. Kupendekeza namna ya malezi ya vijana ili waweze kuwa wazalishaji katika taifa.
- Xv. Kusimamia uanzishaji wa uendelezaji wa vikundi vya jamii na vya hiari vya wananchi katika Halmashauri kwa mujibu wa sera ya maendeleo ya Jamii.
- Xvi. Kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kila mtoto aliyefikia umri

Kwenda shule anafanya hivyo.
Xvii. Kupendekeza sheria ndogo zinazohusu kamati hizi.